WIZARA YA
ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

HESLB
BODI YA MIKOPO
TUNAWEKEZA KWA KIZAZI CHA BAADAE

# MWONGOZO WA UTOAJI MIKOPO KWA WANAFUNZI WA STASHAHADA (DIPLOMA)

## 2024/2025



## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ACSEE** | Cheti cha Kidato cha Sita |
| **CSEE** | Cheti cha Kidato cha Nne |
| **DMO** | Mganga Mkuu wa Wilaya |
| **NACTVET** | Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| **NIDA** | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa |
| **OLAMS** | Mfumo wa Usimamizi wa Maombi ya Mkopo |
| **RITA** | Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini |
| **RMO** | Mganga Mkuu wa Mkoa |
| **SIPA** | Akaunti ya Kudumu ya Mwanafunzi |
| **TASAF** | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania |
| **WyEST** | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| **ZCSRA** | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |

# 1.0 MAELEKEZO MUHIMU KWA WANAFUNZI WOTE WANAOOMBA MIKOPO

Waombaji wote wa mikopo ya elimu kwa ngazi ya Stashahada kwa mwaka wa masomo **2024/2025** wanafahamishwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Kusoma na kufuata taratibu za maombi katika Mwongozo wa mwaka wa masomo **2024/2025**;

(ii) Kuhakikisha kuwa namba ya mtihani wa Kidato cha Nne atakayoitumia mwombaji iwe sawa na atakayoombea udahili wa chuo;

(iii) Kuhakikisha kuwa fomu ya maombi ya mkopo na mkataba **zimesainiwa** na Viongozi wa Serikali ya Mtaa, Mdhamini na Kamishna wa Viapo;

(iv) Waombaji wajaze fomu zao kwa **ukamilifu** na **kuzisain**i kabla ya kuziwasilisha HESLB kwa njia ya **mtandao;**

(v) Kuhakikisha kwamba vyeti vya kuzaliwa/vifo vimethibitishwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini **(RITA)** au Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar **(ZCSRA).**

(vi) Kwa mwombaji ambaye amezaliwa nje ya nchi na/au mzazi wake aliyefariki nje ya nchi anapaswa kuwasilisha barua kutoka **RITA** au **ZCSRA** kuthibitisha taarifa ya kuzaliwa au kifo.

(vii) Kwa mwombaji mwenye **akaunti ya benki** ajaze taarifa zake kwa usahihi kwenye fomu ya maombi ya mkopo;

(viii) Kwa mwombaji mwenye **Namba ya simu** na **Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA),** ahakikishe anajaza namba hizo wakati wa kuomba mkopo.

(ix) Waombaji wote wanakumbushwa kuzingatia muda wa mwisho wa kutuma maombi kwa njia ya mtandao.

## 2.0 KUFUNGULIWA DIRISHA LA MAOMBI

Kwa wanafunzi wanaotarajia kuomba mikopo ya elimu kwa ngazi ya Stashahada, dirisha la maombi ya mkopo kwa mwaka wa masomo **2024/2025** litafunguliwa kwa kuzingatia udahili wa muhula wa **MACHI NA OKTOBA.** Kwa muhula wa Oktoba dirisha litafunguliwa Kuanzia tarehe **1 Juni, 2024** hadi tarehe **31 Agosti, 2024.**

## 3.0 SIFA STAHIKI

Sheria na Kanuni za Bodi ya Mikopo zinaainisha **sifa na vigezo** vya jumla kwawanafunzi wanaohitaji mkopo baada ya kudahiliwa na vyuo vyenye ithibati. Mwombaji atatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

### 3.1 Vigezo vya Msingi vya Mwombaji Mkopo

(i) Awe Mtanzania mwenye umri usiozidi **miaka 35** wakati wa kuomba mkopo;

(ii) Awe amedahiliwa katika taasisi ya elimu inayotoa elimu ya ngazi ya kati nchini;

(iii) Awe amekamilisha na kuwasilisha maombi ya mkopo kupitia mfumo wa maombi ya mkopo **(OLAMS);**

(iv) Asiwe na ajira au mkataba wa kazi serikalini au sekta binafsi unaompatia mshahara au kipato;

(v) Awe amehitimu elimu ya **Kidato cha Nne (CSEE), Cheti (astashahada)** au **Kidato cha Sita (ACSEE)** ndani ya **miaka mitano**; yaani kati ya mwaka **2020** hadi **2024.**

(vi) Kwa mwanafunzi anayeendelea na masomo ahakikishe matokeo yake yanayomwezesha kuendelea na masomo yametumwa Bodi, kupitia Afisa Mikopo/uongozi wa Chuo.

### 3.2 Hali ya Kijamii na Kiuchumi

(i) Uyatima; aliyefiwa na mzazi au wazazi

(ii) Familia au kaya ya kipato duni inayofadhiliwa na Mifuko wa Maendeleo ya Jamii **(TASAF)** au taasisi nyingine za kitaifa zinazotoa ufadhili kwa kaya zenye vipato duni;

(iii) Ulemavu wa mwombaji au wazazi wake.

# 4.0 UPANGAJI WA MIKOPO

Upangaji wa mikopo utazingatia vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Mwanafunzi mwenye udahili kwenye programu zilizoainishwa na kufafanuliwa katika Kipengele cha **6.0** cha Mwongozo huu;

(ii) Hali ya kijamii kama ilivyofafanuliwa katika kipengele cha **3.2** cha mwongozo huu.

# 5.0 NYARAKA ZA KUAMBATISHA WAKATI WA MAOMBI YA MKOPO

Zifuatazo ni nyaraka muhimu za kuambatisha kwenye maombi ya mkopo: -

(i) Cheti cha kuzaliwa kutoka mamlaka husika, **ZCSRA** kwa waombaji kutoka Zanzibar au **Namba ya Uhakiki** (verification number) kutoka **RITA** kwa waombaji kutoka Tanzania Bara;

(ii) Vyeti vya vifo vya wazazi kuthibitisha **uyatima** kutoka mamlaka husika, **ZCSRA** kwa waombaji waliozaliwa Zanzibar au **Namba ya Uhakiki** (verification number) kutoka **RITA** kwa waombaji waliozaliwa Tanzania Bara;

(iii) Barua kutoka **RITA** au **ZCSRA** kuthibitisha taarifa za kuzaliwa kwa waombaji waliozaliwa nje ya nchi. Kwa mwombaji ambaye mzazi wake amefariki nje ya nchi anapaswa kuwasilisha barua kutoka **RITA** au **ZCSRA** kuthibitisha taarifa za kifo.

(iv) Fomu ya Kuthibitisha Ulemavu wa mwombaji au mzazi wake iliyoidhinishwa na Mganga Mkuu wa Wilaya (**DMO**) au Mganga Mkuu wa Mkoa (**RMO**);

(v) Namba ya kaya ya Mnufaika kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (**TASAF**) kuthibitisha ufadhili wa kiuchumi alioupata mwombaji wakati wa elimu yake ya sekondari.

# 6.0 KOZI HUSIKA KATIKA UTOAJI WA MIKOPO

Katika mwaka wa masomo **2024/2025** mikopo itatolewa kwa wanafunzi waliodahiliwa kwenye Kozi za Kipaumbele katika makundi mawili. Mkopo utatolewa kwa kuzingatia kipaumbele cha kozi na uhitaji wa kitaifa.

## 6.1 Kozi za Kundi la Kwanza

Kundi hili litahusisha wanafunzi waliodahiliwa katika masomo yafuatayo:-

### 6.1.1 Health and allied sciences

Clinical Dentistry, Diagnostic Radiotherapy, Occupational Therapy, Physio therapy, Clinical Optometry, Dental Laboratory Technology, Orthotics & Prosthetics, Health Record & Information, Electrical and Biomedical Engineering, Enviromental Health Sciences, Health Records Information Technology, and Medical Laboratory Sciences.

### 6.1.2 Education and vocational training

Diploma in Education (Physics and any other subject), Diploma in Education (Mathematics and any other subject), Diploma in Teaching (Technical and Vocational Education).

### 6.1.3 Transport and logistics

Aircraft Mechanics, Ship Building and Repair, Railway Construction and Maintenance, Global Logistics and Supply Chain Management, Marine Transport and Nautical Science, Shipping and Logistic Management, Transport and Supply Chain Management, Naval Architecture and Offshore Engineering.

### 6.1.4 Energy engineering, mining and earth science

Renewable Energy Engineering (Hydro, Wind, Solar), Pipeline, Oil and Gas Engineering, Oil and Gas Engineering Technology, Environmental Engineering and Management, Lapidary and Jewelry, Mineral Processing, Geology and Mineral Exploration, Petroleum Geosciences and Exploration, Land and Mine Surveying, Metallurgy and Mineral Processing Engineering, Mining Engineering.

### 6.1.5 Agriculture and livestock

Leather Technology, Food Technology and Human Nutrition, Sugar Production Technology, Sugarcane Production Technology, Veterinary Laboratory Technology,

Horticulture, Irrigation Engineering na Agro Mechanization.

**6.2 Kozi za Kundi la Pili**
Kundi hili litahusisha wanafunzi waliodahiliwa kwenye kozi zilizomo kwenye fani zifutazao: **'Energy Engineering', 'Mining & Earth Science',** na **'Agriculture & Livestock'** ambazo hazijatajwa kwenye kundi **6.1**, kipengele cha **6.1.4** na **6.1.5** wanaruhusiwa kuomba mkopo.

# 7.0 VIPENGELE NA VIWANGO VYA MKOPO

Bodi itapanga mkopo kwa viwango vya fedha kulingana namahitaji na ukomo wa bajeti. Mkopo utagawanywa katika vipengele vifuatavyo: Chakula na Malazi, Ada ya Mafunzo, Gharama za Vitabu na Viandikwa, Mahitaji Maalumu ya Kitivo, Gharama za Utafiti na Mafunzo kwa Vitendo.
Mkopo utatolewa kwa ajili ya kugharimia vipengele vyote au baadhi ya vipengele, kama itakavyochambuliwa na kuidhinishwa.

**7.1 Chakula na Malazi**
Kiwango cha juu kisichozidi **TZS. 7,500.00** kwa siku kitatolewa kulingana na idadi ya siku mwanafunzi atakazokuwa chuoni kama inavyoelekezwa kwenye kalenda ya chuo husika. Kiasi hiki kitalipwa moja kwa moja kwa mwanafunzi.

**7.2 Ada ya Mafunzo**
Kiwango cha juu cha ada kisichozidi **TZS. 1,200,000.00** kwa mwaka kulingana na gharama zinazolipwa katika chuo husika kwa mwaka na kitalipwa moja kwa moja kwa chuo husika kama itakavyoidhinishwa na Bodi.

**7.3 Gharama za Vitabu na Viandikwa**
Kiwango cha juu kisichozidi **TZS. 200,000.00** kwa mwaka kwa vitabu na viandikwa na kitalipwa moja kwa moja kwa wanafunzi.

**7.4 Mahitaji Maalumu ya Kitivo**
Kiwango cha juu kisichozidi **TZS. 300,000.00** kwa mwaka kitatolewa na gharama husika zitalipwa moja kwa moja chuoni.

**7.5 Mafunzo kwa Vitendo**
Kiwango cha juu kisichozidi **TZS. 7,500.00** kwa siku hadi siku **56** kwa mwaka, kwa ajili ya Mafunzo kwa Vitendo kitatolewa. Kiasi hicho kitalipwa moja kwa moja kwa mwanafunzi.

### 7.6 Gharama za Kazimradi

Kiasi cha juu kisichozidi **TZS. 100,000.00** kwa mwaka kitatolewa na kulipwa kwa mwanafunzi kwa baadhi ya programu kama zilivyoainishwa na chuo husika.

# 8.0 MASHARTI MENGINE

### 8.1 Wajibu wa Mdhamini na Mzazi/Mlezi

Wazazi/Walezi na wadhamini wana wajibu wa kuthibitisha usahihi wa taarifa ambazo zitawasilishwa katika fomu ya maombi ya mkopo kabla ya kusaini. Mdhamini wa mkopo anaweza kuwa mzazi, mlezi au ndugu au watu wanaokubalika kisheria kuwa mdhamini au mtu ambaye si Mwanafunzi mnufaika wa mkopo. Mdhamini atatakiwa kuhakikisha kwamba mkopaji anajaza taarifa sahihi zitakazotumika wakati wa urejeshaji. Aidha mdhamini/Mzazi/Mlezi atatakiwa kutoa taarifa za mkopaji na makazi pale atakapochelewa au kushindwa kurejesha mkopo wake.

Kwa mwanafunzi aliye na umri chini ya **miaka 18** wakati wa kuomba mkopo atalazimika kujaza tamko rasmi (declaration) kuridhia kuendelea kupokea mkopo pindi atakapotimiza umri wa **miaka 18.**

**Mwombaji wa mkopo anapaswa kuambatisha picha (passport size) ya mdhamini na nakala ya kitambulisho kimojawapo kati ya vilivyotajwa hapo chini, ambacho kimetolewa na mamlaka za Serikali ya Jamhuri ya Muungano waTanzania au Serikali ya Mapinduzi Zanzibar:-**

(i) Kitambulisho cha Taifa
(ii) Kadi ya mpigakura
(iii) Leseni ya udereva
(iv) Pasi ya kusafiria
(v) Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi

### 8.2 Urejeshaji Mkopo

Baada ya kuhitimu masomo ya elimu ya kati, mnufaika wa mkopo atatakiwa kurejesha mkopo wake wote kwa makato yasiyopungua asilimia kumi na tano **(15%)** ya mshahara wake wa kila mwezi au kiwango kisichopungua **TZS 100,000.00** kwa mwezi kwa Mnufaika aliyejiajiri kwenye sekta isiyo rasmi. Iwapo mnufaika ataachishwa/atakatisha masomo, mkopo huo wote utalipwa kwa mkupuo. Mikopo yote inatozwa asilimia moja **(1%)** ya ada ya uendeshaji kwenye deni la msingi la mnufaika **kwa mara moja.**

# 9.0 UDAHILI NA KUHAMA CHUO AU PROGRAMU NDANI YA CHUO

Udahili wa wanafunzi wa Stashahada utapokelewa kupitia NACTVET (kwa vyuo vilivyo chini ya NACTVET) na WyEST (kwa vyuo vya Ualimu vilivyo chini ya Wizara).

Endapo Mnufaika wa mkopo atabadilisha programu ya masomo ndani au nje ya chuo chake, mkopo/stahili zake zitahamishwa na HESLB baada ya kupokea uthibitisho wa chuo husika alichohamia. Aidha, HESLB haitafanya malipo kwa wanafunzi ambao watahamia programu ambazo hazijaainishwa katika mwongozo huu.

Uhamisho wa mkopo **hautabadilisha** kiwango cha mkopo kilichopangwa awali, isipokuwa tu pale ambapo mwanafunzi amehamishwa na mamlaka au kama Bodi itakavyoona inafaa.

# 10.0 JINSI YA KUOMBA MKOPO

Maombi yote ya mkopo yatafanyika kupitia Mfumo wa Maombi na Usimamizi wa Mikopo (OLAMS). Waombaji wote wa mikopo **WANAKUMBUSHWA** kutumia namba ileile ya Mtihani wa Kidato cha Nne iliyotumika wakati wa udahili.

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa maombi kwenye mtandao, waombaji watapaswa kupakua nakala za fomu za maombi na mikataba ya mkopo kwenye mtandao, kugonga mihuri sehemu husika, kusaini fomu, kuambatanisha nyarakazinazohitajika na kuwasilisha kurasa zilizosainiwa **(namba 2 na 5)** kwenye fomu ya maombi katika OLAMS.

***Mwombaji anatakiwa kupakua fomu sahihi kwa kuzingatia fomu ya mwombaji aliye na umri chini ya miaka 18 au umri wa miaka 18 na kuendelea.***

# 11.0 ADA YA MAOMBI YA MKOPO

Waombaji wanapaswa kulipia ada ya maombi ya mkopo ya kiasi cha shilingi **elfu thelathini (TZS. 30,000.00)** kwa namba ya kumbukumbu ya malipo wanayoipata katika mfumo na kulipia kupitia **Benki** au kwa mitandao ya **Simu.** Kwa maelezo zaidi tembelea: https://olas.heslb.go.tz

## 12.0 ORODHA YA WATAKAOPANGIWA MIKOPO

Orodha ya wanafunzi watakaopangiwa mikopo itatangazwa kupitia akaunti za **kudumu za waombaji mikopo (SIPA).**

## 13.0 RUFAA DHIDI YA KIWANGO CHA MKOPO

Waombaji ambao hawataridhika na viwango vya mikopo watakavyopangiwa wanaweza kukata rufaa kwa kujaza fomu za rufaa kwenye mtandao kupitia akaunti za kudumu za waombaji mikopo za SIPA**.** Dirisha la Rufaa kwa mwaka 2024/2025 litafunguliwa kuanzia tarehe **15 Septemba, 2024 hadi tarehe 30 Septemba, 2024.**

## 14.0 MAULIZO NA MALALAMIKO

Waombaji walio na maswali wanashauriwa kuwasiliana nasi kupitia Kituo cha Simu cha HESLB (0736 66 55 33); WhatsApp 0739 66 55 33; Mitandao ya Kijamii Iliyothibitishwa yaani X, Instagram na Facebook (HESLB Tanzania) na e-Mrejesho (www.heslb.go.tz)

**Imetolewa na:-**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU**
**JUNI 1, 2024**

**Call Centre +255 736 66 55 33**
**WhatsApp +255 739 66 55 33**

HESLB Tanzania HESLB Tanzania HESLB_Tanzania

#Kazilendelee
#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

## DODOMA

Jengo la PSSSF, Br. Makole, eneo la Uhindini

S.L.P 984, Dodoma

+255 758 067577

+255 739 067577

info@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
1 Mtaa wa Kilimo, Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068,15471
Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Email: info@heslb.go.tz

## ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900,Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Email: zanzibar@heslb.go.tz

## ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712, Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Email: arusha@heslb.go.tz

## MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa ya pili
Br. Kenyatta
S.L.P 3051, mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Email: mwanza@heslb.go.tz

## MBEYA

Jengo la CAG, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Email: mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya pili
S.L.P 969, Mtwara
Simu: 0733 068 171
Email: mtwara@heslb.go.tz